HALMASHAURI YA MANISPAA YA ILEMELA

Mhe. Mwenyekiti,

BARAZA LA MADIWANI

TAARIFA YA MKURUGENZI KATIKA MKUTANO WA BARAZA LA MADIWANI KWA KIPINDI CHA ROBO YA TATU (JANUARI – MACHI) MWAKA WA FEDHA 2024/2025

TAREHE 11/04/2025.

UTANGULIZI

Mhe. Mwenyekiti, Kwa mujibu wa Kanuni za kudumu za Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela za Mwaka 2014, Mkurugenzi anawajibika kulitaarifu Baraza la Madiwani kwa kutoa Taarifa ya Matukio mbalimbali ambayo yamefanyika au yanatarajia kutokea katika kipindi cha kila Robo ya Mwaka. Hivyo, Taarifa hii imegawanyika katika Maeneo yafuatayo: -

1. TAARIFA YA MAKUSANYO KWA ROBO YA TATU
2. UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO ROBO YA TATU

2.1 MAPATO YA NDANI

2.1 Utekelezaji wa Miradi kwa fedha za Mapato ya Ndani Bajeti ya 2024/2025 kwa robo ya tatu

2.2 SERIKALI KUU

2.2.1 Utekelezaji wa Miradi kwa fedha za Serikali Kuu robo ya tatu

3. TAARIFA ZA MATUKIO MBALIMBALI KWA KIPINDI CHA ROBO YA TATU
4. HITIMISHO

1. TAARIFA YA MAKUSANYO KWA ROBO YA TATU

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kwa mwaka wa fedha 2024/2025 Halmashauri yetu imekusudia kukusanya kiasi cha shilingi 14,953,400,000.00 katika bajeti ya mapato ya ndani, ambapo hadi kufikia tarehe 31 Machi mwaka wa fedha 2024/2025 Halmashauri imefanikiwa kukusanya jumla ya shilingi 10,471,802,011 sawa na asilimia 70.03 ya lengo la mwaka. Ambapo kati ya fedha hizi kiasi cha shilingi 7,951,446,763 ni ya mapato yasiyolindwa sawa na 77% ya lengo na kiasi cha shilingi 2,520,335,348 ni mapato lindwa sawa na 54% ya lengo.

2. UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO ROBO YA TATU

2.1 Utekelezaji wa miradi kwa fedha za mapato ya ndani bajeti ya 2024/2025

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa robo ya pili, jumla ya shilingi 834,573,215.66 fedha za mapato ya ndani zilielekezwa kwenye miradi mbalimbali ya maendeleo ikiwa ni utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2024/2025 katika sekta mbalimbali kwa mchanganuo ufuatao;

(a) Sekta ya ujenzi, mipango miji na miundombinu ziliekezwa jumla ya shilingi 280,632,559.00

(b) Sekta ya Elimu msingi zilielekezwa jumla ya shilingi 212,500,000.00

(c) Sekta ya Elimu Sekondari ziliekezwa jumla ya shilingi 92,432,800.00

(d) Sekta ya afya ziliekezwa jumla ya shilingi 80,000,000.00

(e) Sekta ya maendeleo ya jamii ziliekezwa jumla ya shilingi 69,736,006.66

(f) Sekta ya Utawala ziliekezwa jumla ya shilingi 24,996,000.00

(g) Sekta ya usafi wa mazingira na udhibiti wa takangumu ziliekezwa jumla ya shilingi 5,000,000.00

(h) Sekta ya kilimo, biashara na uwekezaji ziliekezwa jumla ya shilingi 39,274,970.00

2.2 SERIKALI KUU

2.2.1 Utekelezaji wa Miradi kwa fedha za Serikali Kuu robo ya tatu

Mheshimiwa Mwenyekiti; katika kipindi hiki fedha zilizopokelewa ni shilingi **1,036,564,468** kutoka Serikali Kuu ambapo shilingi **833,333,333.00** ni kutoka programu ya Green and Smart Cities SASA na shilingi **203,231,135.00** ni kutoka Mfuko wa kunusuru Kaya Maskini (TASAF) kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli mbalimbali za maendeleo.

3. TAARIFA ZA MATUKIO MBALIMBALI KWA KIPINDI CHA ROBO YA TATU.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mnamo tarehe 17/01/2025 Wajumbe wa Kamati ya Taifa ya uongozi ya TASAF Dr. Naftali Ngondi na Dr. Ruth Lugwisha

wakiambatana na wataalam wengine walifika katika Halmashauri yetu ili kufanya Ziara katika miradi inayotekelezwa kwa fedha za TASAF ikiwemo ufugaji wa samaki na ujenzi wa Zahanati ya Mihama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mnamo tarehe 07/02/2025 Jeshi la Zimamoto Wilaya ya Ilemela lilifika katika Halmashauri yetu na kutoa mafunzo juu ya tahadhari katika matumizi ya moto kwa watumishi wa Halmashauri. Pamoja na mambo mengine, Mkuu wa Zimamoto Wilaya alisisitiza kuwa, "Matumizi ya vifaa vya umeme visivyo na ubora vinaweza kusababisha ajali ya moto". Hivyo inapasa kuchukua tahadhari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mnamo tarehe 21/02/2025, Mkuu wa Mkoa wa Mwanza Mheshimiwa Saidi Mtanda alifika katika Halmashauri yetu, Kata ya Shibula kwa ajili ya kutembelea eneo la uwanja wa Ndege lenye mgogoro wa ardhi na kuongea na wananchi wa maendeo hayo. Pamoja na mambo mengine, amewataka wananchi kuendelea kuwa wavumilivu katika kipindi hiki ambacho Serikali inatafuta suluhu ya mgogoro huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mnamo Tarehe 27/02/2025 Halmashauri yetu ilikabidhi spika 19 kwa maafisa maendeleo ya jamii wa kata 19 za Halmashari zilizogharimu jumla ya shilingi 5,700,000.00 fedha za mapato ya ndani ikiwa ni utekelezaji wa agizo la Waziri wa nchi Ofisi ya Rais TAMISEMI, Mheshimiwa Mohamed Mchengerwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mnamo Tarehe 28/02/2025 Halmashauri yetu ilikabidhi mikopo ya thamani ya shilingi 1,135,500,000.00 kwa vikundi 60 vya Wanawake, Vijana na Watu wenye Ulemavu vilivyokidhi vigezo. Katika mchanganuo wa ugawaji vikundi 39 vya Wanawake vilipokea mkopo wa shilingi 618,600,000.00 Vikundi 11 vya Vijana vilipokea mkopo wa shilingi 492,900,000.00 na Vikundi 4 vya Watu wenye Ulemavu vilipokea mkopo wa shilingi 24,000,000.00.

4. HITIMISHO

Tunapenda kutoa shukrani za dhati kwa Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuendelea kutupa fedha kwa ajili ya kutekeleza Miradi mbalimbali ya maendeleo katika Halmashauri yetu, vilevile tunapenda kumshukuru Mhe. Mbunge Dkt. Angelina S. Mabula kwa kuendelea kuchochea na kuhamasisha maendeleo katika Halmashauri yetu, pia tunamshukuru Mhe. Mkuu wa Wilaya ya Ilemela, Waheshimiwa Madiwani, Wenyeviti wa Mitaa, Watumishi wote wa Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela na Wananchi wote kwa ujumla kwa kuendelea kutoa ushirikiano kwa ajili ya kuendelea kutekeleza Miradi ya Manispaa ya Ilemela.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Naomba kuwasilisha.

Ummy M. Wayayu

MKURUGENZI WA MANISPAA YA ILEMELA